

Bajeti Mikopo ya Elimu 2026/2027, Wanafunzi wengi kunufaika

Dodoma, Mei 8, 2026

Wanafunzi zaidi ya 280,000, miongoni mwao, wanafunzi 111,342 wa mwaka wa kwanza, wanatarajiwa kunufaika na ugharimaji wa masomo yao katika vyuo vya kati na vya elimu ya juu baada ya serikali kutenga TZS 1.07 trilioni kwa ajili ya mwaka wa masomo 2026/2027.

Akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali imetenga TZS 1.07 trilioni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu katika mwaka wa fedha 2026/2027.

Kiasi hicho kimeongezeka kwa TZS 84.2 bilioni ikilinganishwa na mwaka 2025/2026 ambapo kiasi cha TZS 916.5 bilioni kilitengwa kwa ajili ya mikopo na ruzuku kuwanufaisha wanafunzi 252,773 ambapo kati yao, wanafunzi 88,000 walikuwa watarajiwa wa mwaka wa kwanza.

Lengo kuu la ongezeko la fedha za ruzuku na mikopo ya wanafunzi ni kupanua fursa za wanafunzi wenye sifa kujiunga na vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu nchini.

Serikali imeeleza kuwa uwekezaji huo utaendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu, hususan kwa wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini, huku ukichochea upatikanaji wa wataalamu katika sekta mbalimbali muhimu za maendeleo ya taifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia, amesema sehemu ya fedha hizo pia zinalenga kugharimia wanafunzi 2,738 watakaonufaika na 'Samia Scholarship' katika mwaka wa masomo 2026/2027, kati yao, wanafunzi 1,000 ni wa mwaka wa kwanza.

Licha ya kuongeza bajeti ya mikopo, serikali imesema itaendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa mikopo ya wanafunzi ili kuhakikisha fedha zinawafikia walengwa kwa wakati, kuongeza uwazi katika mchakato wa maombi na kuboresha usimamizi wa marejesho ya mikopo kwa wahitimu.

Kuongezeka kwa bajeti ya mikopo na ruzuku za wanafunzi kupitia HESLB kunatarajiwa kuwa kichocheo muhimu katika kuongeza idadi ya vijana wanaopata elimu ya juu, kuimarisha nguvu kazi yenye ujuzi na kuunga mkono juhudi za serikali za kujenga uchumi wa kisasa unaotegemea maarifa, sayansi na teknolojia.

Serikali imeendelea kuonesha dhamira yake ya kuhakikisha Watanzania wengi wanapata fursa ya elimu ya juu kwa kuongeza fedha za mikopo kupitia HESLB mwaka hadi mwaka.

Kupitia bajeti ya mwaka 2026/2027, ni uthibitisho kuwa uwekezaji katika elimu ya juu si matumizi ya kawaida, bali ni uwekezaji wa moja kwa moja katika maendeleo ya rasilimali watu kwa mustakabali wa Taifa.



JAMBO
LETU

Jaqueline Msuya
Mhariri

Msimu mpya mikopo 2026/2027 umeanza...

• Unaomba mkopo? Zingatia mwongozo

Ndoto za maelfu ya vijana wa Kitanzania wanaotarajia kujiunga na vyuo vya elimu ya juu na vya kati zimeanza kupata mwanga kufuatia kufunguliwa rasmi kwa dirisha la maombi ya mikopo kwa mwaka wa masomo 2026/2027. Hatua hii inaashiria mwanzo wa safari muhimu kwa wanafunzi wanaotegemea mikopo ya elimu kugharimia masomo yao na kufanikisha malengo yao ya kitaaluma.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imefungua dirisha la maombi ya mikopo kuanzia Juni 19, 2026 na linatarajiwa kufungwa Agosti 31, 2026, ikimaanisha litakuwa wazi kwa siku 73.

Kipindi hiki kinawalenga wanafunzi wanaotarajia kujiunga na vyuo vya elimu ngazi ya kati (stashahada) na elimu ya juu (shahada) katika mwaka wa masomo unaotarajiwa kuanza mwishoni mwa Oktoba 2026.

Waombaji wanaostahili ni pamoja na wahitimu wa kidato cha nne, kidato cha sita, vyeti na stashahada waliomaliza masomo yao ndani ya kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2022 hadi 2026.

Pamoja na kufunguliwa kwa dirisha la maombi, HESLB ilizindua Miongozo ya Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka wa masomo 2026/2027. Miongozo hiyo ilizinduliwa Juni 19, 2026 na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, ikiwa na lengo la kuwapa waombaji taarifa sahihi kuhusu masharti, vigezo na utaratibu wa kuomba mikopo.

Miongozo minne (04) iliyozinduliwa ni wa Utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Shahada za Awali (Bachelor Degree), Utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Stashahada (Diploma), Utoaji Mikopo kwa Stashahada ya Juu ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo (Postgraduate Diploma in Legal Practice), na Mwongozo wa Utoaji Ruzuku za Samia (Samia Scholarship).

Kupitia miongozo hiyo, waombaji wanapaswa kuelewa kwa kina sifa za kustahili mkopo, namna ya upangaji wa viwango vya mikopo kulingana na hali ya kijamii na kiuchumi pamoja na mahitaji ya programu za masomo wanazotarajia kudahiliwa.

Kwa miaka mingi, changamoto kubwa imekuwa si upatikanaji wa fursa za kuomba mkopo bali ni baadhi ya waombaji kushindwa kujaza maombi yao kwa usahihi kutokana na kutofuata maelekezo yaliyomo kwenye mwongozo husika.

Ili kuokoa muda na kuepuka makosa yanayoweza kuathiri maombi, waombaji wanashauriwa kusoma mwongozo na kuhakikisha wanakuwa na nyaraka zote muhimu kabla ya kuanza kujaza fomu za maombi mtandaoni.

Miongoni mwa nyaraka hizo ni namba ya utambulisho wa cheti cha kuzaliwa (BVN), picha ya pasipoti ya mwombaji pamoja na ya mdhamini wake (mzazi au mlezi), na kitambulisho. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na Kitambulisho cha Taifa (NIDA) na Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Waombaji wanatakiwa kujaza maombi yao kupitia mfumo wa mtandao wa HESLB (OLAS), ambapo taarifa zote binafsi, za kielimu na za wazazi au walezi huwasilishwa kwa njia ya kidijitali.

Kwa mwaka wa masomo 2026/2027, HESLB inatarajia kuona ongezeko la waombaji watakaokamilisha maombi yao kwa usahihi na kwa wakati. Hata hivyo, mafanikio hayo yatawezekana tu iwapo waombaji watachukua muda wa kusoma mwongozo, kuandaa nyaraka zote muhimu na kufuata hatua zote zinazohitajika katika mfumo wa maombi.

Kwa wanafunzi wanaotamani kujiunga na elimu ya juu, ujumbe ni mmoja tu, soma mwongozo, andaa nyaraka zako mapema na wasilisha maombi yako kabla ya Agosti 31, 2026. Hii ndiyo hatua ya kwanza kuelekea kutimiza ndoto zako za elimu na maisha ya baadaye.

NDANI...



03
TAHLISO:
Daraja Muhimu
Wanafunzi na HESLB



07
Alipochagua
Ufugaji Nyuki,
Wengi Walimshangaa Simulizi ya
Mwanafunzi Anayevunja Mipaka



Mwenyekiti
Dkt. Bill Kiwia

Katibu
Amani Kakana

Mhariri
Jaqueline Msuya

Wajumbe
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Ramadhan Namaru

Designer
Saiki Visual Arts
+255 621 579 833

Mawasiliano
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

Simu:
+255 758 067 577
+255 739 067 577

Barua pepe:
info@heslb.go.tz

Tovuti:
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



HESLB Yapanua Wigo Huduma, Ushirikiano wa Kimkakati

Dodoma, 19 Mei, 2026

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imepiga hatua muhimu kupitia ushirikiano wa kimkakati na taasisi mbalimbali za umma unaolenga kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza uelewa wa kifedha kwa wanufaika wa mikopo ili kuendelea kutekeleza dhamira yake ya kuwawezesha wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Miongoni mwa mafanikio ya hivi karibuni ni uzinduzi wa programu ya elimu ya fedha kwa wanafunzi wa elimu ya juu uliofanyika Mei 18, 2026 kwa kuzindua ushirikiano rasmi kati ya HESLB na Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Uzinduzi huo uliofanyika jijini Dodoma katika Ofisi za Makao Makuu ya BOT, ulishuhudiwa na wanahabari, na kuongozwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na viongozi hao wawili wa taasisi za umma, Programu hiyo inalenga kuwajengea wanafunzi maarifa na stadi za kusimamia fedha kwa ufanisi, ikiwemo kupanga bajeti, kuweka akiba, kutumia mikopo kwa tija, kutumia huduma za fedha kidijitali kwa usalama pamoja na kuelewa haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma za kifedha.

Kupitia mfumo wa Student's Individual Permanent Account (SIPA), wanafunzi watanufaika na maudhui ya elimu ya fedha yatakayowasaidia kufanya maamuzi sahihi ya kifedha wakati wa masomo na baada ya kuhitimu. Mpango huo unaendana na maono ya HESLB ya kujenga kizazi chenye uwajibikaji wa kifedha na uwezo wa kuchangia maendeleo ya taifa.

Hatua hiyo imekuja sambamba na jitihada nyingine za kuboresha upatikanaji wa huduma za mikopo kwa wananchi. Mnamo Aprili 22, 2026, HESLB ilisaini makubaliano ya utekezaji wa ushirikiano na Shirika la Posta Tanzania (TPC) yatakayowezesha utoaji wa huduma za maombi ya mikopo kwa njia ya mtandao kupitia mtandao mpana wa ofisi za Posta zilizopo nchini.

Ushirikiano huo unalenga kuwafikishia huduma waombaji wa mikopo katika maeneo mbalimbali ya Tanzania kwa urahisi zaidi, huku wakihakikishiwa upatikanaji wa mtandao wa Internet na msaada wa kitaalamu katika hatua za maombi. Kwa kuwa TPC ina mtandao mpana wa ofisi zaidi ya 350 nchini, huduma hiyo inatarajiwa kuongeza urahisi, usalama na ufanisi kwa waombaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Kwa zaidi ya muongo mmoja, HESLB na TPC zimekuwa zikishirikiana katika kurahisisha huduma kwa wanafunzi. Makubaliano haya mapya yanaendeleza ushirikiano huo kwa kuzingatia mahitaji ya sasa ya matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa umma.

Ushirikiano wa hivi karibuni kati ya HESLB na BOT katika utoaji wa elimu ya fedha pamoja na ule wa HESLB na TPC katika kuboresha upatikanaji wa huduma za maombi ya mikopo unaonesha dhamira ya Bodi ya kuendelea kuboresha uzoefu wa wanafunzi katika safari yao ya elimu. Kupitia ubunifu, matumizi ya teknolojia na ushirikiano na wadau mbalimbali, HESLB inaendelea kutekeleza jukumu lake la kuwezesha vijana wa Kitanzania kufikia ndoto zao za elimu ya juu na kuchangia maendeleo na uchumi wa taifa.






KISHINDO AWAMU YA SITA: HESLB YAVUNJA REKODI 2025/2026

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2021/2022-2025/2026) ambacho Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa madarakani, HESLB imevunja rekodi kwa kuweza kukusanya mikopo iliyoiva yenye thamani ya **TZS 955.15 bilioni** ikilinganishwa na **TZS 949.61 bilioni** zilizokusanywa ndani ya miaka 15 kuanzia **2006/2007 - 2020/2021**".

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia.

MLINGANISHO KATI YA MIAKA 15 YA MWANZO NA MIAKA MITANO ILIYOPITA





TAHLISO:

Daraja Muhimu Wanafunzi na HESLB

Dar es salaam, Jumatano 24 Juni, 2026

Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) imeendelea kuwa kiungo muhimu kati ya wanafunzi na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ikiwa ni jitihada za kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya juu wanapata huduma bora za mikopo na taarifa sahihi kuhusu ufadhili wa masomo yao.

Katika mazungumzo maalum na Jarida la HESLB Yako, Rais wa TAHLISO Geofrey Kiliba anaeleza kuwa umoja huo umejikita katika kuhakikisha sauti za wanafunzi zinasikika na changamoto zao zinawasilishwa kwa mamlaka husika kwa lengo la kuboresha mazingira ya kujifunzia na ustawi wao kwa ujumla.

Anasema TAHLISO, kupitia viongozi wa serikali za wanafunzi katika vyuo mbalimbali nchini, imekuwa ikiratibu ukusanyaji wa maoni, changamoto na mapendekezo yanayowasilishwa na wanafunzi, hususan wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

"TAHLISO ni mwavuli unaunganisha serikali za wanafunzi nchini. Tunapokea changamoto kutoka kwa viongozi wa wanafunzi katika vyuo mbalimbali na kuzifikisha kwa wadau husika ikiwemo HESLB ili zipatiwe ufumbuzi kwa wakati," anasema Kiliba.

Kwa mujibu wa Mhe. Kiliba, ushirikiano uliopo kati ya TAHLISO na HESLB umechangia kwa kiasi kikubwa kuwafikisha wanafunzi taarifa sahihi kuhusu masuala ya mikopo, ikiwemo taratibu za maombi, rufaa, uhakiki wa taarifa na wajibu wa wanufaika.

Anabainisha kuwa kila mwaka viongozi wa wanafunzi hushiriki katika kutoa elimu kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ili kuwawezesha kuelewa kwa usahihi miongozo inayotolewa na HESLB.

"Tunawahamasisha wanafunzi kufuatilia taarifa kutoka vyanzo rasmi na kusoma kwa makini miongozo inayotolewa. Mara nyingi changamoto nyingi zinazojitokeza husababishwa na kutokuzingatia maelekezo wakati wa kujaza maombi ya mikopo," anaeleza.

Katika mazungumzo hayo, Mhe. Kiliba anasisitiza umuhimu wa wanafunzi kutumia viongozi wao kama njia ya kufikisha changamoto zinazowakabili badala ya kutegemea taarifa zisizo rasmi ambazo wakati mwingine huweza kuwapotosha.

Aidha, anaeleza kuwa TAHLISO imeendelea kuwa mshirika wa karibu wa taasisi mbalimbali zinazohusika na maendeleo ya elimu ya juu nchini kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira bora ya kujifunzia na huduma zinazokidhi mahitaji yao.

Kwa upande wake, Jarida la HESLB Yako linatambua mchango wa TAHLISO katika kuimarisha mawasiliano kati ya HESLB na wanafunzi. Kupitia mtandao wake wa viongozi katika vyuo mbalimbali, umoja huo umeendelea kusaidia kufikisha taarifa muhimu kwa wanufaika wa mikopo na kurahisisha upatikanaji wa mrejesho kutoka kwa wanafunzi.

Kadri idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu inavyoendelea kuongezeka kila mwaka, nafasi ya TAHLISO kama daraja kati ya wanafunzi na HESLB inaendelea kuwa muhimu zaidi. Ushirikiano huu unatarajiwa kuendelea kuimarika kwa manufaa ya wanafunzi na maendeleo ya sekta ya elimu ya juu nchini.

Kwa mtazamo wa wengi, mafanikio ya utoaji wa mikopo hayaishii katika upatikanaji wa fedha pekee, bali yanahusisha pia uwepo wa mifumo madhubuti ya mawasiliano na ushirikiano. Katika eneo hilo, TAHLISO imeendelea kuthibitisha nafasi yake kama mdau muhimu anayechangia ustawi wa wanafunzi wa elimu ya juu Tanzania.



“KIDUCHU FRESH TUNASONGA”

**Yaongeza Fursa Wanufaika
Kurejesha Mikopo kwa Urahisi**



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, tarehe 17 Aprili, 2026 alizindua rasmi kampeni ya urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu itwayo “KIDUCHU FRESH TUNASONGA” kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), zilizopo Dar es Salaam.

Kampeni hiyo inalenga kuwahamasisha wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, hususan waliopo katika sekta isiyo rasmi na wenye kipato cha chini, kuanza kurejesha madeni yao kwa kiasi kidogo kuanzia TZS 5,000/= kulingana na uwezo wao wa kifedha hadi watakapomaliza kulipa deni lote.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Wanu alisema Serikali imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika elimu ya juu ili kuwawezesha vijana wengi Zaidi wa kitanzania kufikia ndoto zao za elimu na maendeleo.

“Kiduchu ni kidogo ya kidogo, na upekee wake ni kuwafikia wanufaika wenye kipato cha chini ili waweze kurejesha mikopo yao kulingana na uwezo wao. Msisubiri hadi muwe na fedha nyingi; anzeni na kiduchu mlichonacho leo,” alisema Mhe. Wanu.

Aliongeza kuwa urejeshaji wa mikopo ni msingi wa uendeleu wa mfuko wa elimu kwani fedha zinazorejeshwa huwasaidia wanafunzi wengine kupata mikopo na kuendelea na masomo yao.

Kampeni ya “KIDUCHU FRESH TUNASONGA” inalenga kuwafikia wanufaika 135,186 wanaodaiwa zaidi ya TZS 920 bilioni ambao bado hawajaanza au wamekwama katika urejeshaji wa mikopo yao kutokana na changamoto mbalimbali za kiuchumi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, Prof. Hamisi Dihenga, alisema kampeni hiyo imejengwa katika misingi ya utu na kuzingatia hali halisi ya maisha ya wanufaika. “Kazi na Utu imetufikisha hapa ili tuwafikirie wanufaika wenye kipato cha chini. Watu hatulingani, hivyo ni muhimu

kutoa fursa inayozingatia uwezo wa kila mmoja,” alisema Prof. Dihenga.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alisema kampeni hiyo ni mwendelezo wa mikakati ya kuimarisha urejeshaji wa mikopo baada ya kampeni za “Sifurisha” na “Fichua”, na kwamba sasa HESLB inalenga kuwafikia wanufaika ambao wana nia ya kulipa lakini uwezo wao wa kifedha ni mdogo.

Katika kuhakikisha ujumbe wa kampeni hiyo unawafikia wananchi wengi zaidi, HESLB ilifika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge ili wawe mabalozi wa kampeni hiyo katika majimbo yao. Kupitia ushiriki huo, wabunge walipata fursa ya kufahamu malengo ya kampeni na umuhimu wa kuwahamasisha wanufaika wa mikopo kuanza kurejesha madeni yao kwa kiwango wanachomudu.

Miongoni mwa viongozi waliotembelea banda la HESLB ni pamoja na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Dkt. Pius Chaya, ambaye alipongeza juhudi za HESLB za kutoa elimu kwa umma kuhusu maombi na urejeshaji wa mikopo.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge walitoa maoni na ushauri mbalimbali wakisisitiza umuhimu wa kuongeza utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu taratibu za maombi ya mikopo na urejeshaji wake huku wakihimiza HESLB kuendelea kutumia vyombo vya habari, maonesho na majukwaa ya kijamii kufikisha elimu kwa wananchi wengi zaidi.

Kupitia kampeni ya “KIDUCHU FRESH TUNASONGA”, HESLB inaendelea kuimarisha utamaduni wa urejeshaji wa mikopo kwa njia rahisi, nafuu na jumuishi. Kampeni hiyo inatoa fursa kwa kila mwanufaika kuchangia kulingana na uwezo wake, huku ikihakikisha mfuko wa mikopo unakuwa endelevu ili kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi wa sasa na wa baadaye kufikia ndoto zao za elimu ya juu.



HESLB, CRDB Bank, Wadau Wawajengea Uwezo Waombaji Mikopo

Dar es Salaam, Jumatatu, Juni 22, 2026

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kushirikiana na Benki ya CRDB na wadau wengine wa kimkakati, imefanikiwa kutoa elimu ya uombaji mikopo kwa maelfu ya wanafunzi wanaotarajia kujiunga na elimu ya juu katika mwaka wa masomo 2026/2027 katika mikoa 12 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa upande wa Tanzania Bara, zoezi hilo lilifanyika kuanzia tarehe 20 hadi 29 Mei, 2026 katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Arusha, Mtwara, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Tabora na Kagera. Baada ya kukamilika kwa awamu hiyo, HESLB ilielekea Zanzibar ambapo elimu hiyo ilitolewa katika visiwa vya Pemba kuanzia tarehe 1 hadi 3 Juni, 2026 na baadaye Unguja kuanzia tarehe 8 hadi 12 Juni, 2026.

Programu hiyo iliyowafikiwa wadau zaidi ya 10,000, iliwalea wanafunzi wahitimu wa kidato cha sita wanaotarajia kuomba mikopo, wazazi, walezi pamoja na wadau wa elimu kwa kuwapatia uelewa sahihi kuhusu taratibu za uombaji wa mikopo, maandalizi ya nyaraka muhimu, ujazaji sahihi wa maombi, pamoja na wajibu wa urejeshaji wa mikopo baada ya kuhitimu masomo.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Meneja wa HESLB Kanda ya Arusha, Bi. Lucy Kirigha, alisema kuwa lengo la programu hiyo ni kuhakikisha waombaji wote wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu mchakato wa maombi ya mikopo ili kupunguza makosa yanayoweza kujitokeza wakati wa uwasilishaji wa maombi.

Alisema elimu hiyo imekuwa muhimu katika kuwajengea uwezo wanafunzi, wazazi na walezi ili kuandaa mapema nyaraka zinazohitajika na kufuata taratibu zote za maombi kwa usahihi na kwa wakati.

Benki ya CRDB ilikuwa moja wa wadau wakuu walioshirikiana na HESLB kuandaa na kutoa huduma za kifedha katika maeneo yote yaliyofikiwa. Kupitia ushirikiano huo, wanafunzi walipata fursa ya kufungua akaunti za benki ambazo ni miongoni mwa mahitaji muhimu katika mchakato wa maombi ya mikopo na upokeaji wa fedha za mikopo wanapokuwa chuoni.

Wadau wengine wa kimkakati walioshiriki katika utoaji wa elimu na huduma mbalimbali ni Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Idara yake inayohusika na Anwani za Makazi (NaPA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shirika la Posta Tanzania (TPC) pamoja na Kampuni ya simu YAS. Taasisi hizo zilitoa huduma za uthibitishaji wa taarifa, ushauri, upatikanaji wa nyaraka muhimu na huduma nyingine zinazowasaidia waombaji kukamilisha maombi yao kwa urahisi zaidi.

Mafanikio ya programu hiyo yalibainishwa kupitia maoni ya wanafunzi walionufaika na elimu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini. Akizungumza wakati wa zoezi la utoaji elimu lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya (CUoM), mwanafunzi aliyehitimu kidato cha sita mwaka huu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Songea (Songea Girls' Secondary School), Bi. Grace

Michael Mnkabenga, alisema ameridhishwa na namna HESLB na taasisi inazoshirikiana nazo zilivyoweza kusogeza karibu huduma kwa wananchi.

"Nimefurahi sana kupata elimu na huduma kutoka katika taasisi mbalimbali kwa wakati mmoja. Hii imetupunguzia usumbufu wa kuzunguka kutafuta huduma kutoka taasisi hizi muhimu, hasa kwa sisi tunaotarajia kuomba mikopo hivi karibuni. Kipekee tunaishukuru HESLB kwa kuweza kutusogeza huduma hizi karibu kupitia ushirikiano na wadau wake wa kimkakati," alisema Grace.

Kauli hiyo inaakisi mafanikio ya mkakati wa HESLB wa kupeleka huduma karibu na wananchi na kuwapa waombaji fursa ya kupata huduma zote muhimu zinazohusiana na maombi ya mikopo katika eneo moja kwa wakati mmoja.

Sambamba na utoaji wa elimu kwa waombaji wapya wa mikopo, HESLB pia ilitumia jukwaa hilo kutoa elimu kuhusu umuhimu na taratibu za urejeshaji wa mikopo kwa wanufaika waliomaliza masomo yao, ili kuimarisha uelewa kuhusu wajibu wa kila mnufaika katika kuhakikisha mfuko wa mikopo ya wanafunzi unakuwa endelevu na kuwafikia wataanzania wengine wanaohitaji msaada wa kifedha kuwawezesha kumudu gharama za masomo ya elimu ya juu.

Ushirikiano kati ya HESLB, Benki ya CRDB na wadau wengine wa kimkakati umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kufanikisha na kuimarisha upatikanaji wa elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi kwa wanafunzi watarajiwa wa vyuo vya kati na vya elimu ya juu.

Alipochagua Ufugaji Nyuki,

Wengi Walimshangaa Simulizi ya Mwanafunzi Anayevunja Mipaka

Dar es salaam, Jumatano 24 Juni, 2026

Kwa wengi, ufugaji nyuki ni shughuli inayohitaji ujasiri mkubwa. Taswira iliyozungukwa na maelfu ya nyuki huwatisha watu wengi, pamoja na yote, hali hii imekuwa chachu kwa msichana mdogo aliyeanza safari yake ya elimu ya juu. Faith Meleck, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam anayesomea Shahada ya Sayansi katika Ufugaji Nyuki, hofu hiyo haikuwa sababu ya kuachana na ndoto zake.

Faith ametokea katika familia yenye kipato cha chini kijiji cha Nronga kilichopo mkoani Kilimanjaro. Maisha ya familia yake yalitegemea kilimo cha kujikimu, huku wazazi wake wakijitahidi kwa hali na mali kuhakikisha watoto wao wanapata elimu.

“Tangu nikiwa mdogo nilikuwa na ndoto ya kuwa mtaalamu wa afya ili niweze kusaidia jamii yangu kupata huduma bora za matibabu. Nilijitahidi sana masomoni licha ya changamoto nyingi nilizokutana nazo. Mara nyingi nilisoma kwa mwanga wa kandili kutokana na ukosefu wa umeme nyumbani, lakini sikuacha kuamini kuwa elimu ndiyo njia ya kubadilisha maisha yangu na ya familia yangu”, anasema Faith.

Baada ya kufaulu vizuri kidato cha sita, nilichaguliwa kujiunga na chuo kikuu kusomea Shahada ya Sayansi ya Ufugaji Nyuki. Furaha yangu ilikuwa kubwa, lakini changamoto mpya ilijitokeza, gharama za ada, malazi, chakula na vifaa vya masomo zilikuwa kubwa kuliko uwezo wa familia yangu. Niliona ndoto yangu ikiwa hatarini kutotimia.

Anasema hapo ndipo Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilipokuja kuwa mwanga wa maisha yake. Baada ya kutuma maombi ya mkopo na kufanikiwa kupatiwa fedha za masomo, alipata fursa ya kuendelea na masomo bila vikwazo vikubwa vya kifedha. Mkopo huo ulimwezesha kulipa ada, kununua vitabu, kupata vifaa muhimu vya kujifunzia na kukidhi baadhi ya mahitaji yake ya kila siku chuoni.

Faith anaongeza kuwa kupitia mkopo huo, aliweza kuelekeza nguvu zake katika masomo badala ya kuhangaika kutafuta namna ya kupata fedha za kuendesha maisha chuoni. Anafafanua kuwa alifanya vizuri darasani na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kitaaluma zilizoongeza maarifa na uwezo wake.

“Watu wengi waliniuliza kwa nini nichague kozi ya nyuki wakati kuna kozi nyingine nyingi. Wengine walidhani nitabadilisha mawazo baada ya kuanza masomo,” anasema.

Tofauti na walivyotarajia wengi, Faith aliingia chuoni akiwa na ari kubwa ya kujifunza. Akiwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza, tayari ameanza kupata maarifa ya awali kuhusu tabia za nyuki, umuhimu wao katika mazingira na mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika maendeleo ya uchumi.

Anatanabaisha zaidi kwamba, moja ya mambo yaliyomvutia katika programu hiyo ni fursa zake za kujiajiri pamoja na mchango wake katika uhifadhi wa mazingira.

“Kadiri ninavyoendelea kujifunza ndivyo ninavyogundua kuwa ufugaji nyuki una nafasi kubwa sana katika maendeleo ya jamii. Siyo tu kuhusu asali, bali pia kuhusu biashara, ajira na utunzaji wa mazingira,” anaeleza Faith.

Licha ya kuwa hajafika hatua ya mafunzo kwa vitendo, tayari ameshuhudia baadhi ya shughuli zinazohusisha usimamizi wa mizinga na uzalishaji wa mazao yatokanayo na nyuki. Anakiri kuwa awali alikuwa na hofu kidogo, lakini elimu anayopata chuoni imeanza kubadili mtazamo wake.

Faith ana ndoto ya kuwa mtaalamu wa ufugaji nyuki na kuanzisha miradi itakayowawezesha wanawake na vijana katika jamii yake kunufaika na fursa zilizopo katika sekta hiyo.

Anasema anataka kuwa mfano kwa wasichana wengine wanaoogopa kuchagua fani zinazodhaniwa kuwa ni za wanaume pekee.

“Hakuna kozi ya mwanaume au ya mwanamke. Kilicho muhimu ni kuwa na malengo na kujituma. Mimi bado niko mwaka wa kwanza, lakini ninaamini siku moja nitakuwa miongoni mwa wataalamu watakaobadilisha mtazamo wa jamii kuhusu fani hii,” anasema.

Hivi sasa akiwa anajiandaa na msimu mpya wa mwaka wa masomo 2026/2027, anasema familia yake inaiona nuru ambayo hapo awali ilionekana kuwa mbali sana. Anabainisha kuwa wazazi wake wana furaha kubwa kuona mtoto wao akitimiza ndoto ambayo ilionekana haiwezekani kutokana na hali ngumu ya kiuchumi.

Kwa hakika, HESLB imekuwa daraja la mwanga wa mafanikio ya Faith na kwa maelfu ya wanafunzi wengine kutoka familia zenye kipato cha chini kama yeye. Kupitia mikopo ya elimu ya juu, ndoto zao zimepewa nafasi ya kukua na hatimaye kuonesha njia ya kutimia kwa siku za usoni kuelekea mafanikio.



KAMERA YETU



Aprili 17, 2026, Dar es Salaam: Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir (katikati), akizindua kampeni ya "Kiduchu". Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB, Prof. Hamisi Dihenga, na kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia.



Aprili 17, 2026, Dar es Salaam: Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir (katikati), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB, Prof. Hamisi Dihenga (kushoto), na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia (kulia), wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa HESLB, mara baada ya uzinduzi wa kampeni ya "Kiduchu".



Aprili 17, 2026, Dar es Salaam: Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, akihutubia kabla ya kuzindua rasmi kampeni ya "Kiduchu", inayolenga kuhamasisha na kuelimisha wanufaika wa mikopo wenye kipato cha chini kurejesha mikopo yao kidogo kidogo, ili kuimarisha uendeleu wa Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Juu nchini.



Aprili 22, 2026, Dar es Salaam: Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia (kushoto), akipeana mkono na Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Bw. Macrice Mbodo (kushoto), mara baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano yatakatayowezesha utoaji wa huduma za maombi ya mikopo kwa wanafunzi nchini kupitia mfumo wa mtandao.



Mei 18, 2026, Dodoma: Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba (kushoto), na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia (kulia), wakionesha hati za makubaliano ya ushirikiano (MoU) mara baada ya kusaini makubaliano hayo yatakatayowezesha utoaji wa elimu ya fedha kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini.



Juni 3, 2026, Tanga: Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia (kushoto), na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), CPA Fahad Sudi Hamid (kulia), wakionesha hati za makubaliano ya ushirikiano kupitia mpango wa "Cash Waqf" unaolenga kuongeza vyanzo vya fedha kwa ajili ya kufadhili elimu ya juu nchini.



Juni 30, 2026, Dar es Salaam: Bi. Miriam Farjala (kulia) afisa wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), akihoa elimu ya uombaji sahihi wa mikopo kwa mdau wa elimu, katika programu ya utoaji wa elimu kwa umma.

WASILIANA NASI:

DODOMA

Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la
Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712, Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa
ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

MBEYA

Jengo la CAG, Ghorofa ya
Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya tatu,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu
na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo, Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,
15471-Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

